**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Telegram: **"MLF"**
Simu: +255 26 2322610
Nukushi: +255 262322613 2861908
E-Mail: ps@mlf.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Michezo,
S.L.P. 2870,
**DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

**UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA TAASISI YA UTAFITI WA MIFUGO TANZANIA (TALIRI)**

***Dodoma, Agosti 01, 2026***

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemteua **Prof Esrom D. Karimuribo** kuwa **Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)** kwa kipindi cha pili cha miaka mitatu kuanzia tarehe 20 Julai, 2026.

Aidha, kufuatia uteuzi huo, Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwa mamlaka aliyonayo chini ya Kifungu 8(1) – (2) cha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) ya mwaka 2012, ameteua **Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)** kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia tarehe 20 Julai, 2026 kama ifuatavyo:-

1. Amemteua **Bw. Ombeni Julius Msangi** ambaye ni Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi Mstaafu wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha.
2. Amemteua **Dkt. Esther Gwae Kimaro** ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi, Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST).
3. Amemteua **Dkt. Bugwesa Zablon Katale** ambaye ni Mkurugenzi wa Uratibu na Uendelezaji wa Tafiti wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).
4. Amemteua **Dkt. Caroline Leonard Sichalwe** ambaye ni Afisa Utafiti Mwandamizi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

5. Amemteua **Dkt. Asimwe Lovince Rwiguza** ambaye ni Mkurugenzi wa Nyanda za Malisho na Maendeleo ya Rasilimali za Chakula cha Mifugo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

6. Amemteua **Dkt Stella Francis Bitanyi** ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu, Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania (TVLA).

7. Amemteua **Dkt. Hassan Ally Mrutu** ambaye ni Afisa Mtafiti Mkuu Daraja la I Mstaafu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

8. Amemteua **Bw. Edson Enos Mfuru** ambaye ni Meneja wa Kampuni ya URUS Tanzania Ltd.

**Imetolewa na:-**
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**